**Kwenda:** EXD

**KK:** DRISS

**Kutoka:** DIF

**Tarehe:** 22 Februari, 2023

YAH: **MABORESHO YA MFUMO WA KUSHUGHULIKIA MIRADI**

Katika kutekeleza mojawapo ya majukumu ya Idara ya Huduma kwa wawekezaji TIC inao mfumo ambao kwa upande wa usajili miradi mfumo huu hupokea na kuchakata maombi ya kupata vyeti vya vivutio kwa miradi mipya pamoja na kufanya mabadiliko mbalimbali katika vyeti hivyo.

Mfumo huu umejengwa na wataalam wa ndani na umekuwa katika matumizi kuanzia mwezi Machi, 2020 kwa kuwezesha uchakati wa ndani (Evaluation) kufanywa kwa mfumo na baadaye mwaka 2021 mfumo ulitolewa nje na kuwawezesha wawekezaji wenye maombi kuwasilisha/kuwasiliana na kielektroniki. Mfumo umesaidia kuboreha huduma ya vyeti tangu wakati huo hasa kufupisha muda wa utoaji huduma hiyo.

Hata hivyo zipo changamoto kadhaa zilizojitokeza ambazo Idara ya Huduma na wawekezaji wanakabiliana nazo katika kutumia mfumo. Aidha, kuna masuala yaliyojitokeza ikiwepo kutungwa kwa Sheria mpya ya Uwekezaji, 2022 ambapo yapo maswala yanahitaji kubadilishwa kwenye mfumo. Kutokana na sababu hizo, Idara imepokea kutoka kwa watumiaji wa ndani na baadhi ya wawekezaji na kuorodhesha kwa lengo la kuziwasilisha ili zifanyiwe kazi na wataalam.

Ili kupata mrejesho zaidi baada ya wawekezaji kuutumia mfumo wa nje kwa muda wa miaka miwili, pia napendekeza TIC aindae kikao cha wadau cha kimtandano ili TIC kutoa wasilisho la mfumo huu na kupokea mapendekezo kutoka kwao kwa ajili ya maboresho zaidi. Hivyo, naleta kwako ombi la kuanza mchakato wa uboreshaji wa mfumo wa kushughulikia miradi wa kielektroniki, kwa ajili ya kitengo cha Tehama kufanyia kazi maboresho hayo.



Revocatus Rasheli

DIF

**Changamoto na mapendekezo ya maboresho ya mfumo huu (Ndani-Evaluation) ni kama ifuatavyo:-**

| Na. | Changamoto | Mapendekezo ya maboresho |
|---|---|---|
| 1. | Kuoanisha mfumo na Sheria mpya ya Uwekezaj, 2022 | Mfumo uweze kuingiza maboresho yote yaliyowekwa kwenye Sheria mpya ya uwekezaji 2022<br><br>(i) kutambua miradi inayoomba cheti kwa ajili ya upanuzi (Expansion) na kuweka eneo la kupokelea taarifa za hesbabu zilizokaguliwa kwa miaka mitatu iliyopita (Audited Financial Statements)<br>(ii) Kutengeneza njia ya usajili wa miradi ukarabati wa mradi (Rehabilitation)<br>(iii) Kupungua kwa kigezo cha mtaji ya mradi (threshold) kwa wawekezaji wa ndani wakati wa usajili kutoka dola 100,00 mpaka dola 50,000<br>(iv) Cheti cha vivutio cha mfumo kirejee vifungu vipya vya Sheria ya Uwekezaji 2022 mfano usajili ni kifungu cha 19 sio cha 17 kama ilivyokuwa hapo awali |
| 2. | Kutokuwepo kwa dirisha la huduma kwa wateja (Aftercare) | Mfumo uweze kuongeza dirisha la huduma kwa wateja (Aftercare) ambalo litasaidia wawekezaji wajaze maendeleo ya mradi wake (Progress report) kila baada ya miezi 6 na watajaza Changamoto wanazopata pindi ikitokea. Mwekezaji atapata email ya kumkumbusha kujaza Progress report ikifika tu miezi 6. Hii itasaidia kupata taarifa sahihi za wawekezaji wetu. Lakini pia itatupa taarifa ya changamoto za wawekezaji ili kuzifanyia kazi kwa haraka |
| 3. | Miradi kuonesha kuwa ulipokelewa TIC kabla ya mwekezaji kufanya malipo. TIC inalalamikiwa kuchelewesha maombi ambayo bado hayajaingia TIC | Officially, mradi utakuwa umepokelewa TIC baada ya malipo kufanyika na kuingia kwenye evaluation.<br><br>Kwa usajili wa miradi mipya, maombi yaweze kuonyesha siku ya kupokelewa TIC ni siku ambayo atakuwa mwekezaji amelipia na taarifa zake za malipo zimefika kwenye mifumo yetu. Kwa sasa maombi yanahesabiwa yameingia TIC tarehe ambayo mwekezaji ataingiza nyaraka zake kwenye mfumo hata kama atakuwa hajalipia kutokana na kutokamilisha nyaraka au sababu nyingine. |
| 4. | Taarifa (Report) ya amendments mbalimbali za miradi | Mfumo uweze kutengeneza taarifa na kutenganisha miradi mipya (New application),maombi ya kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi na mabadiliko (Extension na Amendments nyingine). |
| 5. | Kutokuwepo kwa nyaraka za miradi iliyosajiliwa kabla ya mfumo kuanza kutumika | Mfumo uweze kuonyesha Nyaraka zilizoambatanishwa wakati wa maombi ya mwekezaji kwa miradi iliyosajiliwa kabla ya kuanza kwa mfumo huu. |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Mfumo hauhifadhi cheti kilichotolewa kwa mradi | Mfumo uweze kuhifadhi Cheti kwenye mradi husika na watendaji waweze kuona cheti hicho pindi wakihitaji kwa utendaji wao. Kwa sasa cheti kikitoka hakuna nakala inayobakia kwenye mfumo. |
| 7. | Kwenye hatua Evaluation), maafisa hawaoni maoni ya meneja, DIF, ikiwa mradi hautarudi kwake kwa kuchakata upya | Mapendekezo/Maelekezo yanayotolewa wakati wa uchakataji miradi kwa kila hatua, watendaji waweze kuona kwa ajili ya kujifunza na kutorudia makosa yale yale kila wakati. |
| 8. | Kupotea kwa miradi ambayo imekuwa “deferred” zaidi ya mara mbili (2) | Pamoja kumrudisha maombi kwa wawekezaji ili warekebishe yapo maombi ambayo yanarudishwa bila kufanyiwa marekebisho husika hivyo kutakiwa kurudishwa tena kwa mwekezaji. Kwa miradi iliyokuwa “deferred” zaidi ya mara mbili (2), hupotea kwenye mfumo bila kujulikana ulipo na kuna muda mwingine unaonekana kwa mwekezaji lakini haoni maelekezo aliyotumiwa na DIF, hivyo kushindwa kujua ni nini anatakiwa kufanya na mradi huo unakuwa haupo kwa inbox ya DIF, hivyo kusababisha kuchukua muda mrefu kumaliza uchakataji wa mradi. Mfumo uweze kumuonyesha Mwekezaji endapo atatumiwa maelekezo ya DIF Zaidi ya mara 2. |
| 9. | Mfumo unahifadhi nyaraka (attachments) zikiwa na namba ambazo zinazalishwa na mfumo wenyewe, ikiwa afisa atabadilisha jina la nyaraka na kuziondoa namba zilizozalishwa kwa mfumo, inasababisha mwekezaji kushindwa kusoma tena nyaraka zake iwapo mradi utarudishwa kwake (deferred) | Mfumo uweze kutambua na kuweka nyaraka kwa majina yake halisi. Mfano mwekezaji akiingiza nyaraka kwenye eneo la business plan basi mfumo upokee na kuhifadhi kwa jina la business plan hata kama nyaraka hiyo imepatiwa jina jingine na mwekezaji. |
| 10. | Mfumo unaonyesha sekta ndogo zinazohusu sekta zote za uzalishaji hata kama sekta inayohusika ni moja tu | Mfumo uoneshe sekta ndogo zinahihusiana na sekta mama tu |
| 11. | Mfumo hautoi taarifa pale mradi unapoingia kwenye akaunti ya meneja au Mkurugenzi. (Notification) | Mfumo uweze kutoa taarifa (notification) kwa watendaji pindi mradi ukiingia kwenye akaunti husika hasa Maneja, DIF na EXD. Taarifa inaweza ikatumwa kwa email kama ilivyo kwa e office. |
| 12. | Mfumo kutotofautisha nyaraka zilizotumwa mwanzoni wakati wa maombi na nyaraka zilizorudishwa kwenye mfumo baada ya marekebisho (Deferement). | Baada ya DIF “kudeffer” mradi, Mfumo unatakiwa uonyeshe utofauti wa nyaraka zilizowasilishwa kielekroniki na mwekezaji baada ya kufanya marekebisho, zikiwa tofauti na zilizotumwa mwanzoni. (Re-submitted) |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Changamoto ya kuwa na miradi iliyofanyiwa kazi lakini bado inaonekana kwenye akaunti za evaluators (Officers, Manager, DIF na EXD) | Miradi iliyokwishafanyiwa kazi iondolewe kwenye akaunti za watendaji. Mfano ipo miradi 40 ya amendment kabla ya malipo (Imeambatishwa) ambayo ilishafanyiwa kazi na hata kutoa CoI ila bado imebaki kwenye akaunti ya DIF |
| 14. | Changamoto ya Mradi uliofanyiwa kazi na mtendaji mmoja na kupelekwa kwa mtendaji mwingine kuonyesha tarehe ya nyumba (created date) | Miradi ukiwa umefanyiwa kazi na mtendaji mmoja na kupelekwa kwa mtendaji mwingine, uonyeshe tarehe ya siku ulipokwenda na sio kuonyesha tarehe za nyuma (created date) |
| 15. | Kwa miradi ya "Extension" DIF akimpelekea afisa/manager kwa ajili ya kufanyia kazi na afisa akafanyia kazi na kumrudishia, mfumo bado unaonyesha taarifa za DIF za awali wakati anamuelekeza afisa huyo, na DIF anapopeleka kwa EXD bado maelekezo ya awali yanakuwa kwenye eneo lake la kuandika taarifa, hivyo kupelekea DIF aidha afute au aandike kwa chini | Kwa upande wa extension tuomba maboresho yafanyike kwa ujumla maana eneo hilo halikufanyiwa kazi kwa undani. |
| 16. | Maombi ya amendment eg extension yakiwa nje kabla ya malipo yakirudishwa kwa mwekezaji na DIF bado mradi unabaki kwa DIF. Hakuna uhakika kama mradi umerudi kwa mwekezaji | Maombi ya amendment yanaporudishwa kwa mwekezaji ili kurekebisha yaondoke ka DIF |
| 17. | Options za maamuzi ya DIF kwenye evaluation ya maombi ya amendments "Submit for" | Evaluation window kwa ajili ya amendment wakati mradi ukiwa nje kabla ya malipo iweke option ya "assign officer" badala ya PVV kwa kuwa DIF anaweza ku assign kwa kazi zingine sio PVV peke yake |
| 18. | Maombi ya amendment ya **extension** maneno ya "Investors Reasons" | Yabadilishwe na na badala yake yawekwe "Reasons for Project Implementation Delay" ili wawekezaji waweze kueleza sababu za kuchelewa kukamilika miradi |

**Changamoto na mapendekezo kwa mfumo (Nje -Wawekezaji)**

| Na. | Changamoto | Mapendekezo |
|---|---|---|
| 1. | Mfumo hauonyeshi "size" ya ukubwa wa attachment inayotakiwa kuwekwa kuingizwa kwenye mfumo | Mfumo uonyeshe ukubwa wa attachment (Max size allowable) linalotakiwa kuwekwa ili kusaidia mwekezaji aweke nyaraka zake kulingana na ukubwa unaotakiwa |
| 2. | Kwenye sehemu ya kuweka nyaraka, eneo la" business plan" imejirudia mara mbili | Marekebisho yafanyike kwa kuweka eneo moja tu la Business plan |
| 3. | Mwekezaji anapomaliza kujaza taarifa ya "page" moja wakati wa kwenda "page" ya pili inaweza kuleta error lakini haionyeshi error imetokana na tatizo gani. | Ni vizuri mfumo unapotoa taarifa ya "error" ionyeshe kuwa hiyo "error" imesababishwa na nini. Aidha, kama ni tatizo la mtandao mfumo useme ni tatizo la mtandao. |
| 4. | Mfumo unaruhusu mwekezaji afungue akaunti zaidi ya moja kwa kampuni moja, ambayo inasababisha kumletea shida wakati wa kuingiza taarifa zake | Mfumo unatakiwa uruhusu Mwekezaji afungue akaunti moja tu kwa kampuni, na kama amesahau password basi afanye maombi kwa kutumia mfumo na mfumo uweze kureset password yake kwa kutumia uthibitisho wa email/phone namba aliyoweka awali. |
|  |  |  |